# HOTUBA YA MWENYEKITI WA TPAWU TAIFA WAKATI WA UFUNGUZI WA SEMINA NA KIKAO CHA TATHMINI NA MIPANGO NA MAKATIBU WA KANDA NA SEHEMU – OKTOBA 2025

---

- **Ndugu Katibu Mkuu TPAWU Taifa,**
- **Makatibu wa Kanda na Sehemu kutoka kanda zetu zote nchini,**
- **Wawakilishi kutoka Makao Makuu,**
- **Wageni waalikwa, mabibi na mabwana,**

**Salamu na Shukrani:**

Nakusalimuni kwa jina la mshikamano na utetezi wa haki za wafanyakazi.

TPAWU………

Kwa niaba ya kamati tendaji TPAWU Taifa, na kwa niaba yangu binafsi, naomba kuchukua fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa lakini pia kwa fahari ya uongozi, kuwakaribisha kwa moyo wa dhati kwenye semina itakayofanyika leo na kikao muhimu kitakachofanyika kesho cha tathmini ya kazi zetu za mwaka uliopita na upangaji wa mikakati ya mwaka ujao. Nitumie fursa hii kuwashukuru nyote kwa kuitikia wito wa kushiriki katika

shughuli hii ambayo ina umuhimu mkubwa siyo tu kwa ustawi wa TPAWU bali pia kwa mustakabali wa wafanyakazi wa sekta ya kilimo na mashamba nchini.

Mambo haya yanafanyika katika kipindi muhimu ambapo chama chetu kinaendelea kukua, kuimarika, na kuchukua nafasi yake stahiki katika kutetea haki za wafanyakazi wa sekta ya kilimo na mashamba nchini Tanzania.

Ndugu zangu, Kabla ya kuendelea mbele, nichukue nafasi hii kuwapongeza nyote – Makatibu wa Kanda, makatibu wa sehemu, na wanachama wetu wote – kwa kazi kubwa na ya kujituma mliyoifanya kwa kipindi cha mwaka mzima. Ingawa mwaka huu haukukosa changamoto, mmeonesha mfano wa kuigwa katika uongozi, usimamizi wa haki za wafanyakazi na kuendeleza mshikamano wa ki-undugu baina ya wanachama. Kwa dhati kabisa, nawapongeza kwa kazi kubwa, ya kujitolea, mnayoifanya katika kanda zenu. Hali ya mazingira ya kazi katika sekta ya kilimo haijawahi kuwa rahisi. Lakini bado mmeendelea kusimama imara, mkiongoza kanda zenu, mkiwatetea wanachama wetu, na mkiendeleza imani ya wafanyakazi kwa TPAWU.

**Pongezi za kipekee** ziende kwa Katibu Mkuu na timu nzima ya sekretarieti kwa uthabiti wenu katika kuratibu shughuli zote za kiutendaji za makao makuu ya chama, na kusaidia kanda zetu kufanya kazi kwa ufanisi.

**Lengo na Umuhimu wa Semina na Kikao hiki:**

Semina ya leo na Kikao chenu cha kesho vimeitishwa kwa madhumuni ya kuongeza uelewa na ujuzi, kutathmini utekelezaji wa majukumu tuliyojiwekea kwa mwaka 2024/2025, pamoja na kupanga mikakati ya mwaka wa 2026.

Katika kikao chenu, mtutakuwa na nafasi ya kujadili kwa kina:

- Utekelezaji wa majukumu katika kanda zetu
- Changamoto zilizojitokeza
- Mafanikio yaliyopatikana
- Na namna ya kuboresha huduma zetu kwa wanachama wetu

Ni muhimu kufanya tafakari ya kina na kwa uwazi ili kujenga msingi imara wa utendaji wetu wa baadaye.

**Kaulimbiu ya Mwaka: Kiongozi Mwadilifu Ni Nguzo ya Maendeleo**

Mwaka huu tumejiwekea kaulimbiu inayoakisi kiu ya wanachama wetu na mwelekeo wa chama chetu. Naomba nirudie kwa msisitizo:

**“CHAGUA VIONGOZI WAADILIFU, WENYE MAONO NA WELEDI KWA MAENDELEO YA TPAWU”**

Kaulimbiu hii ni mwongozo wa maamuzi yetu, ni kioo cha dhamira ya chama chetu. Tunapaswa kuhakikisha kuwa kila chaguzi zinazoendelea – kuanzia ngazi ya tawi hadi taifa – zinafuata msingi huu. Kiongozi mwadilifu si yule anayejitangaza kwa nguvu, bali anayejenga kwa mfano, anayesikiliza, anayeheshimu wanachama, na anayelinda maslahi ya wengi.

**Tathmini ya Kazi na Mafanikio:**

Kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, baadhi ya mafanikio ambayo tunapaswa kujivunia kama chama ni pamoja na:

- **Kuongeza usajili wa wanachama wapya**, hasa kutoka maeneo ambayo awali yalikuwa na changamoto ya uhamasishaji.
- **Kutoa elimu ya kisheria na haki za kazi kwa wanachama wetu**, kupitia semina, makongamano na warsha zilizoendeshwa katika kanda mbalimbali.
- **Kuimarisha ushirikiano kati ya chama na waajiri** katika baadhi ya mashamba makubwa na sehemu nyingine za kazi, ambapo sasa tunashirikishwa kikamilifu katika masuala ya mazingira ya kazi.
- **Kuwakilisha wanachama wetu katika mashauri ya kikazi** na kuhakikisha wanapata haki zao kwa mujibu wa sheria.

Haya si mafanikio ya mtu mmoja, bali ni matokeo ya juhudi za pamoja kutoka kwa viongozi wote wa ngazi mbalimbali – kutoka makao Makuu, Kanda, Sehemu hadi Matawini. Hii yote ni ishara kuwa chama kinazidi kupata nguvu na kuaminiwa.

## Changamoto Zilizojitokeza:

Pamoja na mafanikio hayo, bado tumekumbana na changamoto mbalimbali zikiwemo:

- **Upungufu wa rasilimali fedha**, unaokwamisha utekelezaji kamili wa baadhi ya mipango.
- **Ukuaji wa ajira zisizo rasmi**, hali inayowanyima wafanyakazi wengi ulinzi wa kisheria.
- **Uelewa mdogo wa baadhi ya wanachama kuhusu haki zao**, jambo linalohitaji kuimarisha elimu ya uraia na haki kazini.
- **Vikwazo kutoka kwa baadhi ya waajiri**, wanaopinga shughuli za vyama katika maeneo yao ya kazi.

Hatuwezi kufumbia macho changamoto hizi. Badala yake, ni lazima tuzibadilishe kuwa fursa za kujifunza na kuwa wabunifu zaidi katika kazi zetu.

## Mchakato wa Uchaguzi wa Viongozi wa Chama:

Ndugu watendaji wa chama hiki,

Mwaka huu wa 2025 ni mwaka wa uchaguzi wa **viongozi wa matawi** ya chama kote nchini. Zoezi hili ni msingi wa uhai wa demokrasia ndani ya TPAWU. Naomba kusisitiza kuwa uchaguzi huu uendeshwe kwa mujibu wa **katiba ya chama**, kwa uwazi, haki na utulivu.

Kadhalika, mwaka ujao 2026, chama kitaendesha **uchaguzi wa ngazi ya Kanda na Taifa.** Zoezi hili linahitaji maandalizi ya kina kuanzia sasa ili kuhakikisha kuwa tunapata viongozi bora, waadilifu, wenye weledi, na maono ya kukiongoza chama chetu katika karne hii ya 21.

Naomba kutoa rai kwa wanachama wote kuwa sehemu ya mchakato huu kwa kuzingatia kaulimbiu yetu ya mwaka: **"Chagua Viongozi Waadilifu, wenye maono na weledi kwa Maendeleo ya TPAWU."**

Tuwe waangalifu, waadilifu, na waaminifu katika kusimamia mchakato huu. Tuchague viongozi kwa kuzingatia **sifa, uwezo, maadili na dhamira ya kweli**. Tuwe mfano wa kuigwa.

Natoa wito kwenu watendaji: **Tulinde heshima ya chama chetu kwa kusimamia uchaguzi wenye amani, haki na uwazi.** Tujiepushe na makundi ya upendeleo, ubaguzi na migawanyiko isiyo ya lazima. Tuwe wamoja katika kujenga chama chetu.

**Mwelekeo wa Mwaka Ujao (2026):**

Miongoni mwa maeneo ya kipaumbele tutakayoyazingatia mwaka ujao ni:

- Kuendelea na **kampeni za usajili wa wanachama wapya**, hususan katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa vya kutosha.
- Kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa **mikataba ya Hali bora** kwa wafanyakazi na waajiri na kuhimiza mikataba hiyo ifungwe kwenye matawi ambayo haipo na kuhuisha iliyopo.
- Kuimarisha **mafunzo kwa viongozi**, hasa wale wanaochaguliwa upya katika matawi, kanda na taifa.
- Kukamilisha ujenzi wa **mfumo wa taarifa wa kidijitali wa wanachama**
- Kuongeza sauti ya TPAWU katika mijadala ya kitaifa kuhusu mustakabali wa ajira katika sekta ya kilimo.
- Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mikataba ya pamoja katika maeneo yenye ushirikiano rasmi na waajiri.

**Wito kwa Makatibu wa Kanda na Sehemu:**

Makatibu wa kanda na Sehemu, nyie ndio uti wa mgongo wa utekelezaji wa shughuli za chama chetu. Naomba melewe kuwa, ushindi wa chama hiki hautegemei wingi wa maneno, bali unategemea mshikamano, uadilifu, na utendaji unaolenga maendeleo ya pamoja. Ni lazima tushikamane kama familia moja yenye dira moja. Tuongozeni tugombanie nafasi za uongozi kwa heshima,

hoja na uadilifu. Tuwe na mioyo ya kujitolea na kuwa mstari wa mbele katika kutetea maslahi ya wanachama wetu.

Pia, naomba mzingatie yafuatayo:

- Kuendelea kuimarisha mawasiliano baina ya Matawi, Sehemu, Kanda na Makao Makuu
- Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kimaelewano kati ya TPAWU, Waajiri na Wafanyakazi.
- Kuweka utaratibu mzuri wa uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa majukumu yenu kwa wakati
- Kusimamia matawi kwa weledi na maadili
- Kuwa walezi wa viongozi wapya wanaochaguliwa

**Hitimisho:**

Kwa kumalizia, napenda kuwaasa tushiriki semina za leo na kikao cha kesho kwa uzito na umakini. Tuchangie kwa uhuru na ujasiri kwa hoja zenye kujenga, tusikilize kwa uvumilivu, na tuamue kwa hekima. Tuzingatie muda na tuweke mbele maslahi ya chama chetu. Naomba muelewe kuwa tunategemea mabadiliko makubwa sana ya uendeshaji wa chama chetu baada tu ya majadiliano katika semina na kikao hiki.

Kwa heshima na taadhima kubwa sasa, **natamka kuwa shughuli yetu ya siku mbili ya semina na kikao cha tathmini na mipango kati ya TPAWU Taifa na Makatibu wa Kanda na sehemu imefunguliwa rasmi.**

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Mungu ibariki TPAWU.**
**Mungu wabariki Wafanyakazi.**
**Mungu ibariki Tanzania.**

**Imetolewa na:**
*Daniel Bariyanka Joachim*
Mwenyekiti wa TPAWU Taifa
Tarehe: 9 Oktoba 2025